USCF CCT TAKWIMU

# NANYAMBA MISSION OUTREACH

## 2025




Follow us on: USCF_CCT TAKWIMU

USCF CCT TAKWIMU
WE SERVE THE LIVING GOD

# Utangulizi




USCF CCT TAKWIMU ni umoja wa wanafunzi tunaomtumikia Mungu katika Chuo cha Takwimu chini ya mwavuli wa CCT, tunaolelewa na Chaplaincy ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Moja ya huduma zetu ni uinjilisti na mission, kama agizo la Bwana wetu Yesu Kristo.

"Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." (Marko 16:15)
Kwa kutii agizo hili, mwaka 2024 mwezi Juni, tulianza mchakato wa kutafuta eneo kwa ajili ya kufanya huduma ya uinjilisti.

Kwa kushirikiana na CCT Chaplaincy ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tuliandaa maombi ya mfungo wa siku saba na hatimaye tukapendekeza mkoa wa , Mtwara kama eneo linalofaa kwa huduma hii. Baada ya utafiti wa awali tulithibitisha kuwa Halmashauri ya Nanyamba kuwa eneo lenye uhitaji wa huduma za kiroho na kijamii, hivyo tulianza maandalizi rasmi.
Ifahamike kuwa hii ilikuwa ni kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa tawi letu, kufanya huduma hii muhimu, tunao ushuhuda mkubwa na tumeuona mkono wa Mungu ukiwagusa watu wengi kupitia kazi yetu ya uinjilisti. Na baadhi ya huduma zimeelezewa kwa picha katika jarida hii, hivyo nikukaribishe kufuatilia pamoja nami.

# Huduma Ya Uinjilisti Wa Nyumba Kwa Nyumba

Katika huduma hii, tulifanikiwa kufanya uinjilisti wa nyumba kwa nyumba kwa siku nne kati ya siku saba za huduma. Uinjilisti huu ulilenga kuwafikishia watu habari njema za Kristo kwa njia ya ushuhuda wa ana kwa ana na usambazaji wa vipeperushi vyenye mafundisho ya Neno la Mungu. Tulipita katika vijiji na mitaa mbalimbali, tukikutana na watu wa rika tofauti, tukiwahimiza kumkaribisha Kristo katika maisha yao na kuimarika kiroho.

Mbali na kuhubiri, tulijitahidi pia kuonesha upendo wa Kristo kwa vitendo kwa kufanya matendo ya huruma, ikiwa ni pamoja na kuwafariji wenye mahitaji maalum, kuwaombea wagonjwa, na kuwatia moyo wenye changamoto za maisha. Kwa neema ya Mungu, tulishuhudia watu wakiguswa na ujumbe wa wokovu, na wengi walipokea sala ya toba na kuamua kumfuata Kristo.

Huduma hii ilitimiza agizo la Bwana Yesu lililo katika Mathayo 28:19-20, linalosema: *"Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*













**Aidha katika huduma hii watu 194 walifikiwa na 97 walimpokea Kristo na kuongozwa sara ya toba.**

# Mkutano Wa Injili Na Semina Ya Neno La Mungu (Crusade)



Katika huduma hii, tulifanikiwa kufanya mkutano mkubwa wa Injili kwa siku zote saba, kuanzia tarehe 16 Februari, kuanzia saa 9:00 alasiri hadi saa 12:30 jioni kila siku. Mkutano huu ulikuwa na ushiriki mkubwa na uliweka mkazo katika kuleta ujumbe wa wokovu kwa njia mbalimbali za kiinjilisti.

Huduma zilizohusika katika mkutano huu ni pamoja na, neno la Mungu (mahubiri), maombi na maombezi, mahubiri kwanjia ya nyimbo (vikundi mbalimbali vya kwaya na waimbaji binafsi walihudumu) pia watu walitoa shuhuda juu ya matendo wanayotendewa na MUNGU.

Mkutano huu ulikuwa na athari kubwa kwa jamii, kwani watu wengi waliguswa na ujumbe wa wokovu, na wengine waliamua kumpokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yao. Tunamshukuru Mungu kwani wagonjwa 47 waliombewa na kati yao 31 walimshuhudi Mungu kuwa amewaponya, pia watu 117 walimpokea kristo na kuongozwa sara ya toba, na mahudhurio ya jumla ya mkutano ilikuwa ni watu wazima 1144 na watoto 267. Mkutano huu ulitimiza neno la Mungu katika *Marko 16:15, linalosema*: *"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkahubiri Injili kwa kila kiumbe."*





# Huduma Ya Kutoa Elimu Mashuleni




***Huduma hii ilitimiza neno la Mungu katika Methali 22:6, linalosema: "Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha hata atakapokuwa mzee."***

Katika kipindi kizima cha uinjilisti, tulipata fursa ya kutoa huduma ya elimu katika Shule ya Msingi Nanyamba na Shule ya Sekondari Dinyecha, yenye madaraja ya O-Level na A-Level. Huduma hii ilijikita katika kuelimisha na kuhamasisha wanafunzi kuhusu maadili mema, umuhimu wa elimu, na thamani ya kumtumikia Mungu katika safari yao ya masomo.

Aidha, washirika kutoka Chuo cha Takwimu walijitolea kufundisha masomo ya darasani kwa siku zote za huduma, hali iliyopokelewa kwa shukrani na walimu wa shule hizo, kutokana na upungufu wa walimu uliopo katika taasisi hizo.



Vilevile, wanafunzi walifurahia sana uwepo wetu shuleni, si tu kwa ajili ya elimu ya darasani, bali pia kwa sababu ya mafundisho ya kiroho yaliyowajenga kiimani na kuwahamasisha kufuata njia sahihi maishani. Aidha wanafunzi 1534 walihudumiwa katika huduma hii.



# Huduma Ya Matendo Ya Huruma Hospitali

Katika kipindi kizima cha huduma ya Uinjilisti, tulibahatika kufanya huduma ya matendo ya huruma katika Kituo cha Afya Mt. Hildegard Nanyamba, ambapo tuliwatembelea wagonjwa, kuwapa faraja, na kuwaombea. Huduma hii iliwaleta wagonjwa karibu na Mungu, na wengi walifarijika kwa maombi na upendo tuliowaonesha. Katika huduma hii wagonjwa 19 walipewa faraja na maombezi.












## Shuleni

Pia, tulifanikiwa kufanya matendo ya huruma katika shule za msingi na sekondari kwa kugawa vitu mbalimbali kwa wanafunzi wenye uhitaji. Jitihada hizi zilipokelewa kwa shukrani kubwa kutoka kwa walimu, wanafunzi, na wazazi, kwani zilisaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuongeza hamasa kwa wanafunzi. Aidha wanafunzi 1534 walihudumiwa katika huduma hii.

Huduma zote hizi zilitimiza neno la Mungu katika Mathayo 25:35-36 linalosema:

"Kwa maana nalikuwa na njaa, nanyi mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, nanyi mkanipa kinywaji; nalikuwa mgeni, nanyi mkanikaribisha; nalikuwa uchi, nanyi mkanivika; nalikuwa mgonjwa, nanyi mkanijia; nalikuwa kifungoni, nanyi mkanitembelea."

# Siku Maalumu Ya Mfungo Na Maombi

Katika huduma ya Maombi ya Pamoja, timu ya huduma ilitumia siku maalumu ya Ijumaa kama siku ya mfungo na maombi pia kuanzia saa 11:00 alfajiri mpaka saa 4 asubuhi tuliomba kwa ajili ya Nanyamba, Mtwara na Taifa zima,tuliombea pia ukuaji wa makanisa yote yaliyotoa nyoosha mkono katika, mafanikio ya huduma hii.



Maombi yalijumuisha majina ya watu wote walioshiriki katika kufanikisha huduma hii, tuliomba baraka za Mungu ziambatane nao na Mungu akatimize haja za mioyo yao kupitia sadaka zao, pia tuliombea kila mmoja kuhusu masomo yetu, familia zetu, na mahitaji yetu binafsi. Mstari wa Biblia uliotumika ulikuwa "Ombeni bila kukoma" (1 Wathesalonike 5:17).



Timu ilielekea katika eneo tulivu lililozungukwa na mazingira ya amani, katika mtaa wa Nanyamba, ambapo kwa ushirikiano wa uongozi wa CCT Nanyamba na makanisa ya wenyeji eneo hilo lilipatikana.













Eneo hili lilitumika kama sehemu ya kupanda mbegu za maombi, kwa lengo la kuinua maombi yote yaliyofanyika na kuyaweka mikononi mwa Mungu kwa ajili ya baraka na mafanikio ya huduma hii.

# Huduma Ya Uinjilisti Kwa Njia Ya Sinema



Katika kipindi chote cha uinjilisti, tulifanikiwa pia kufanya huduma ya uinjilisti kwa njia ya sinema kila siku kuanzia saa 12:30 jioni hadi saa 2:00 usiku. Huduma hii ilipokelewa vyema na watu wengi, kwani iliwezesha kufikisha ujumbe wa Injili kwa njia ya picha na filamu zenye mafundisho ya Neno la Mungu.

Sinema hizo zilihusisha simulizi za Kibiblia, ushuhuda wa maisha, na mafundisho kuhusu wokovu na maisha ya Kikristo. Filamu zilizoonyeshwa ziliambatana na maelekezo kutoka kwa mkalimani kutoka Idara ya IT ya USCF CCT TAKWIMU, ambaye alihakikisha watazamaji wanapata ufahamu sahihi wa ujumbe uliomo katika filamu hizo.

***Huduma hii ilitimiza neno la Mungu katika Zaburi 96:3, linalosema: "Tangazeni utukufu wake kati ya mataifa, maajabu yake kati ya watu wote."***







# Bonanza La Michezo

Katika huduma ya uinjilisti, tulifanikiwa kuandaa Bonanza la Michezo kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba. Bonanza hili lilianza na jogging kwa washirika wote wa mission, wafanyakazi wa Halmashauri, na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

Michezo mbalimbali ilifanyika, ikiwa ni pamoja na kuvuta kamba, mashindano ya kula, mpira wa wavu, netball, na mpira wa miguu. Michezo hii ililenga kuimarisha umoja, kusherehekea upendo, na kufungua njia ya mawasiliano bora kati ya jamii, serikali, na washirika wa uinjilisti.

Aidha, kama sehemu ya kusherehekea upendo na kudumisha uhusiano, USCF CCT TAKWIMU iligawa zawadi za vifaa vya michezo kwa washirika wa mission, jambo lililothibitisha upendo wa Kristo na mshikamano miongoni mwa washiriki wote. Bonanza hili lilithibitisha umuhimu wa mshikamano na ushirikiano, huku likileta furaha na kutimiza maono ya kudumisha uhusiano wa kidugu katika Kristo.

**Aidha katika huduma hii watu 312 walihudhuria bonanza hilo.**

# Huduma Za Jamii Na Kazi Za Mikono

Katika huduma ya Maombi ya Pamoja, watu walishiriki katika kazi nyingi, ikiwa ni pamoja na mapishi, usafi, na kazi za mikono. Hii ilionesha ushirikiano na upendo mkubwa baina ya washirika, kila mmoja akichangia kwa njia yake mwenyewe. Ushirikiano huu ulileta umoja na nguvu katika kufanikisha huduma, na kila mmoja alionyesha karama aliyopewa na Mungu katika maeneo tofauti. Kazi hii ilileta furaha na mshikamano katika huduma yote.
"Kwa maana kwa neema tuliyopewa, kila mmoja aishi kwa kadiri ya kipawa alichopewa." (Warumi 12:6)










# Shukrani Na Hitimisho




Ashukuriwe Mungu, Muumba wa mbingu na dunia, kwa wingi wa fadhili na neema zake zisizo na kipimo, kwa kutuwezesha kama USCF CCT TAKWIMU kuandaa huduma hii ya uinjilisti na mission mkoani Mtwara, kama lilivyo agizo la Bwana wetu Yesu Kristo katika Marko 16:15 – "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."

Tunamshukuru Mungu kwa kutuletea watu waliotoa michango yao ya hali na mali ili kufanikisha huduma hii. Ikumbukwe kuwa "Fedha ni jawabu la mambo yote" (Mhubiri 10:19), na imeandikwa pia kwamba "Imebarikiwa miguu ile iletayo Habari Njema" (Warumi 10:15)—hata hivyo, wataendaje wasipopelekwa? Michango yao imekuwa baraka kubwa kwa kazi ya Mungu.

Kipekee tunawashukuru waumini na washarika wa CCT UDSM Chaplaincy chini ya Mch. Kiongozi James Lubadanja kwa maombi, michango, na ushauri wao. Pia tunawashukuru wazee wa kanisa, wachungaji viongozi, na baraza la wazee kwa kuturuhusu kutembelea makanisa yao na kupata sapoti kubwa katika huduma hii. Kwa uchache, tunatambua mchango mkubwa wa makanisa haya: CCT UDSM Chaplaincy, KKKT Usharika wa Changanyikeni, KKKT Usharika wa Mbezi Beach, KKKT Usharika wa Kariakoo, KKKT Usharika wa Msasani, KKKT Usharika wa Mbezi Louis, KKKT Usharika wa Mwenge, KKKT Usharika wa Msewe, AICT Pastorate ya Changanyikeni, AICT Pastorate ya Kibaha, AICT Pastorate ya Mbezi Louis, AICT Kanisa la Kiaskofu Magomeni. Makanisa haya yamefanyika baraka kubwa kwetu, na tunathamini sana mchango wao.



Shukrani za pekee pia kwa ndugu Paul kutoka KKKT Kariakoo kwa sadaka yake, ambayo imewezesha kwa kiwango kikubwa mafanikio ya huduma hii, Tunawashukuru pia kwa dhati wana USCF CCT TAKWIMU wote kwa moyo wao wa kushiriki katika maombi, michango, na kwa muda waliotoa kushiriki katika kila hatua ya mchakato huu, hata wakati wa kwenda kuchangisha. Ushiriki wao umeleta nguvu kubwa katika kuendeleza huduma ya Mungu.

kuwa hii imekuwa awamu ya kwanza kwa USCF CCT TAKWIMU kufanya huduma hii, lakini kwa hakika tumemuona Mungu akitenda makuu. Tumepata ushuhuda wa wazi kwamba "Bwana ndiye mchungaji wetu, hatutapungukiwa na kitu" (Zaburi 23:1). Kwa msingi huu, tunaomba ushirikiano wenu kwa wakati mwingine, maana bado lengo letu ni kuzidi kumtangaza Kristo kwa mataifa yote. Tunaomba wasiache kutuwezesha kwa hali na mali ili tuendelee kueneza Injili kwa viwango vikubwa zaidi katika siku za usoni.

***Mwisho, tunamaliza kwa neno la Mungu kama ilivyoandikwa katika***
***1 Wakorintho 15:58 "Basi, ndugu zangu wapendwa, muwe imara, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua ya kuwa taabu yenu siyo bure katika Bwana."***
***Mwisho wa huduma hii ni mwanzo wa maandalizi ya huduma nyinginezo nyingi zijazo tunaomba tuzidi kushirikiana kumtangaza kristo kwa pamoja wakati mwingine USCF TAKWIMU tunawapenda sana mnaweza kutufuatilia zaidi katika mitandao ya kijamii instagram, tiktok na youtube kupata taarifa zaidi na video na matukio zaidi ya mission MUngu awabariki.***



# Kipekee tunawashukuru wafuatao na kuzidi kuwaombea kwani tuliungana nao kwenda kupeleka huduma hii Nanyamba Mtwara




Follow us on: USCF_CCT TAKWIMU

1. ELIKANA LAZARO (CAPTAIN)
2. TUMAIN HOSEA (CAPTAIN)
3. DENIS LUHENDE (CAPTAIN)
4. BARAKA FRANCIS (KATIBU)
5. EZEKIA MWAIPAJA
6. ANNA KIBONA
7. MACHA MARIO
8. WIKAMA SAMSON
9. EMERTHER ONESMO
10. DOTO SAMWEL
11. JANI SHERIA
12. EDWARD LUTTA
13. GILBERT GEORGE
14. DIANA MICHAEL
15. DAVIS CHARLES
16. DENIS BENSON
17. DITRAM HAULE
18. AGRIPPINA CHIDAYA
19. IRENE JOHN
20. EVANSIA KIMARO
21. SAMSON SOSPTER
22. LAZARO MSIGWA
23. NELSON WILSON
24. HELLEN MATEE
25. LUCAS DAUD
26. ROGATE JOHANESS
27. ESTER MGANA
28. DANIEL E WANDWI
29. NEEMA MLIMI
30. SOSTENES J GAMBO
31. MATHAYO MALAGESI
32. ANNE SAMSON
33. BEATRICE LUHANGA
34. DAVIS MARIKI
35. EDSON ELIAKIM
36. HILDA MAEDA
37. KELVIN LAZARO
38. ANITHA MIHAYO
39. JUDITH NUHU
40. JOYCE PHISSOO
41. MAGRETH ANDREA
42. WITNES JOHN
43. RACHEL RICHARD
44. DEUS ILAKOZE
45. ASIA ELISANTE
46. MARIAM LWESYA
47. MAGRETH ANOLD
48. JUNIOR ANDREW
49. HENDRY H. MARGWET
50. EMMANUEL URIO
51. ANJELA
52. FLAVIAN
53. REHEMA
54. GRACE AMON
55. IZENGO MAGANGA
56. JELIUS HENERICO
57. JOHN SHEDRACK
58. NEEMA JUSTICE
59. ZENICE MINJA
60. MRS MALABA
61. BECKY MBABAZI
62. SETH MGAYA
63. CHRISS
64. LEVINA KANUZI
65. ELIPENDO SONGELAEY
66. OBLYSE
67. KELVIN SAMWEL
68. HONEST SHAYO
69. ELISHA DAUDI
70. CALVIN NGOWI
71. JANETH KISANI
72. MAKULIGA WILLIAM
73. MUSSA MALABA
74. EMMANUEL ALLEN
75. SAMSON JONAS

USCF CCT TAKWIMU
WE SERVE THE LIVING GOD

# NANYAMBA MISSION 2025 ACCOMPLISHED

## Ahsante kwa sapoti na Maombi yenu.

**Huduma iliwafikia jumla ya watu 3,421, ambapo watu 214 walimpokea Kristo na kuongozwa katika Sala ya Toba.**










*Follow us on:* *USCF_CCT TAKWIMU*

*USCF CCT TAKWIMU*
*WE SERVE THE LIVING GOD*